**LEARNING BY EAR - "Girls' Rights"**

**EPISODE 6:**

**Title: Domestic Violence and Corporal Punishment – A Story of Girls' Rights**

**AUTHOR: Njoki Muhoho**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 At FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD**

Narrator - 30s Male
Fatuma - 14 Female
Elder Jacob - 60s Male
Mama Fatuma- 60s female

**SCENE 2 FATUMA'S CLASSROOM**

Narrator - 30s Male
Fatuma - 14 Female
Teacher Halima - 30s female
Class - 14 students

**SCENE 3 PLAYING FIELDS**

Fatuma - 14 Female
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Narrator - 30s Male

**SCENE 4 TEACHER MONA'S OFFICE**

Teacher Mona - 30s Female
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Narrator - 30s Male

**SCENE 5 STAFF MEETING**

Headmaster - 40s Male
3-4 Staff - 30s Male and Females
Narrator - 30s Male
Janet-Social Worker - 30s Female

**SCENE 6 GIRLS PARLIAMENT**

Cheptoo - 15 Female
Ciro - 14 Female
Fatuma - 14 Female
Abdi - 15 Male
Group of students (male, female 12-16)

Narrator

**SCENE 7 FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD**

Elder Jacob - 60s Male
Fatuma - 14 Female
Janet-Social Worker - 30s Female
Narrator - 30s Male

**INTRO**

**01. MUSIC: THEME MUSIC**

| | | |
|---|---|---|
| 02. | **NARRATOR** | Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya 'Learning By Ear'- 'Noa Bongo Jenga Maisha yako', bado katika masuala ya **Haki za Wasichana**. Katika kipindi kilichotangulia, marafiki watatu Ciro, Cheptoo na Fatuma wanajitolea kupigana na ajira ya Watoto. Na katika kipindi cha leo, wasichana hawa wanaitisha kikao cha bunge kujadilia mizozo ya kinyumbani na adhabu ya wanafunzi kutandikwa viboko shuleni. Hebu tuungane nao katika safari hii kufahamu zaidi yanayojiri. |

**SCENE 1: FATUMA'S PARENTS' HOMESTEAD**

**03. SFX: NIGHT SOUNDS. HEAVY APPROACHING STEPS. HARD KNOCKING ON DOOR**

**04. SOUNDS: HEAVY BREATHING.**

| | | |
|---|---|---|
| 05. | **MAMA FATUMA** | (SLEEPY) Nini…Nani.. (SHOUTING) Nani huyo? |

06. **ELDER JACOB** (SHOUTING)Nani huuuyo..! Kwani nani mwengine unayemtarajia wakati kama huu Mama Fatuma? Nyenyenye… Naaani huuuyo. Fungua mlango upesi!. Amka wewe mwanamke!. Amka Goi goi wewe. Ni mimi mumeo hapa,Mzee Jacob… (hiccup..hiccup..) Kwani nani mengine uliyemtarajia?

07. **MAMA FATUMA** Lakini ni usiku sana saa hii..…Sote tumelala… (YAWNS) Haya subiri nakuja..!

**08. SFX: HEAVY KNOCKING**

09. **MAMA FATUMA** (ANGRY)Subiri nakuja jamani!

**10. SFX: DOOR OPENS WITH CREAK**

11. **ELDER JACOB** (SHOUTING) Kwani unachukua muda mrefu wewe Mwanamke!

12. **FATUMA** Mama, Mama, ni nini? Kuna tatizo gani?

13. **ELDER JACOB** Fatuma.. ni wewe Msichana goi goi? Hebu Amka upesi unipakulie Chakula.

14. **FATUMA** Lakini ni usiku Baba!. Chakule ni baridi.

15. **ELDER JACOB** (SHOUTING) Mtoto Mvuvi wewe. Changamka!.Nipe chakula…upesi!. Kiko wapi Chakula (SHOUTING LOUDER).

16. **MAMA FATUMA** Amka binti yangu…, Amka umpashie moto chakula.Huoni Babako ana njaa?

17. **FATUMA** (MURMURING)Kukipasha moto chakula! Au kupika!...Yaani hakuna kulala..hii si… (INTERRUPTS)

**18. <u>SFX: LOUD SLAP</u>**

19. **FATUMA** Waaaggggghhh…. (CRIES)

20. **ELDER JACOB** Wewe huwezi kubishana na mimi! Nenda haraka ukapike chakula..!. Wanawake lazima wawapikie chakula waume zao. Mimi ni Babako. Nyinyi wawili nendeni mletee chakula haraka upesi. Sasa hivi.Mmenisikia?

| | | |
|---|---|---|
| 21. | **NARRATOR** | Akinung'unika na kulia huku akiwa bado na usingizi, Fatuma ampashia Chakula Babake. Ni usiku wa manane na lazima arauke kwenda shule.<br><br>Kofi alilozabwa na Babake bado lamwasha. Lakini kwake si uchungu kama kukose usingizi. Endelea kuwa nasi usikie jinsi anavyokabiliana na hali hii siku inayofuatia. |

**22. BRIDGE MUSIC**

**SCENE 2: FATUMA'S CLASSROOM**

**23. SFX: FURNITURE SOUNDS/pupils chatting**

| | | |
|---|---|---|
| 24. | **CLASS** | Habari ya asubuhi Mwalimu Halima. |
| 25. | **TEACHER Halima** | Ni njema tu wanafunzi, haya ketini. |

**26. SFX: FURNITURE SOUNDS**

| | | |
|---|---|---|
| 27. | **TEACHER Halima** | Fungueni vitabu vyenu munionyeshe kazi niliyowapa kufanya nyumbani. |

**28. SFX: DOOR OPENS**

| | | |
|---|---|---|
| 29. | **TEACHER Halima** | Nani huyu anafika darasani saa hizi. Fatuma kwanini umechelewa.? |

| | | |
|---|---|---|
| 30. | **FATUMA** | Samahani Mwalimu, nimeamka kuchelewa.….! |
| 31. | **TEACHER Halima** | (INTERRUPTING)Eti nini? Umechelewa kwasababu umelala sana mpaka ukajisahau. Mvuvi wewe!Mbona wanafunzi wenzako wote wamefika shuleni mapema? |
| 32. | **FATUMA** | Samahani sana Mwalimu… nililazimika kuu…wajua… |
| 33. | **TEACHER Halima** | Najua nini… ? Kiranja wa darasa.. hebu niletee kiboko.Fatuma lazima ukumbushwe kwamba saa za kufika shuleni ni mapema.! PAUSE |
| 34. | **TEACHER Halima** | (COMMANDING) Njoo hapa...! Nitakuchapa viboko 10 kwa kuchelewa. Na wengine muanze kuhesabu.!! |

**35. SFX: RHYTHMIC CRACKING OF WHIP**

| | | |
|---|---|---|
| 36. | **CLASS** | Moja …. Mbili… |
| **37.** | **FATUMA** | SCREAMS RHYTHMICALLY |

**38. SFX: FADE OUT OF WHIP SOUNDS AND CRIES**

39. **NARRATOR** Fatuma ananza kulia huku mwalimu akiendela kumuadhibu.Anamachungu ya kuadhibiwa shuleni na hata nyumbani pia.

Anasubiri kwa hamu kutoka darasani kwa mapumziko ili kukutana na rafikize Ciro, na  Cheptoo uwanjani kama kawaida kwani anahitaji faraja yao.

**SCENE 3: PLAYING FIELDS**

**40. SFX: School yard**

41. **CHEPTOO** Ciro, Mbona Fatuma anachukua muda mrefu sana kutoka. Muda wa mampuziko utamalizika sasa hivi na turudi darasani.

42. **CIRO** Unajua nini Chepto si kila mtu anatoka haraka darasani kama wewe…. Yule pale anakuja. (SHOUTING) Fatuma, Fatuma.. njoo huku.

43. **CHEPTOO** Hebu muangalie.. anatembea kama *Dubwana*! Labda anasinzia akitembea. (SHOUTING) Wewe.. Fatuma, kwani unasinzia ukitembea?

| | | |
|---|---|---|
| 44. | **CIRO** | Ooh … analia. Fatuma kumetokea nini mbona walia? |
| 45. | **FATUMA** | (BREAKS DOWN CRYING) Nimechapwa viboko.. |
| 46. | **CHEPTOO** | Nani huyo aliyekuchapa viboko twende kumfunza adabu?… Tukiwa wasichana sisi pia tunauwezo wa kumfunza mtu adabu.. |
| 47. | **CIRO** | Cheptoo, si mzaha, anasikia uchungu!. |
| 48. | **FATUMA** | Kila mtu ananipiga, Babangu nyumbani…. na sasa Mwalimu! |
| 49. | **CIRO** | Kwani umefanya nini? |
| 50. | **CHEPTOO** | Wewe …wewe… wewe… Hata masichana afanye kosa gani haki ya kupigwa… Ulimwengu huu uliojaa ukatili, kama wewe ni msichana ni kupigwa tu. |
| 51. | **CIRO** | Na nani? |
| 52. | **FATUMA** | Jana usiku, Babangu, na leo Mwalimu. |
| 53. | **CIRO** | Cheptoo.. Wacha utani, jana ulipigwa ukifanya nini? |

| | | |
|---|---|---|
| 54. | **FATUMA** | Kosa nililotenda ni kudai haki yangu kupewa muda wa kuala wa kati ya saa 6 na 7. Lakini… lakini sikupata. Ilinibidi kuamka usiku kumpikia Babangu aliyefika nyumbani usiku wa manane . Kisha akanipiga….!. Leo mimi na mamangu tumechelewa kuamkau. Na tena kufika shule, Mwalimu ananisubiri na kiboko kwa kufika shuleni kuchelewa. (CRYING)Nimechoka.. Mgongo wangu unaniuma… kwanini wasichana hawawezi kuishi bila kupigwa? |
| 55. | **CHEPTOO** | Lakini kwanza, kwanini Msichana apigwe? Nafikiri wakati umewadia kuitisha kikao cha bunge letu la wasichana. Twendeni kwa Mwalimu Mona atupe ushauri zaidi. |

56. **NARRATOR** Sasa changamoto inayowakumba wasichana hawa ni moja tu. Wanajiuliza ni vipi wanweza kukomesha uovu huu, ikiwa Mwalimu anaweza kutoa adhabu kali kwa wasichana kama ilivyo katika shule nyingi Barani Africa?

Endelea kusikilia wakati Wasichana wanapokutana na Mwalimu Mona ofisni mwake .

**Scene 4 TEACHER MONA'S OFFICE**

**57. SFX: office sounds like people talking in the background, typing, telephone**

58. **TEACHER MONA** Cheptoo, Ciro na Fatuma….mnataka kuniona?..... Kuhusu nini?

59. **CHEPTOO** Mwalimu tunataka kuitisha kikao cha Bunge la wasichana kujadilia masuala ibuka kama vile adhabu ya kutandikwa viboko.Lakini kwanza tumeona tupate ushauri.

60. **TEACHER MONA** Endeleeni nasikiliza!.

| | | |
|---|---|---|
| 61. | **CHEPTOO** | Fatuma alichapwa na Mwalimu alipofika shuleni kuchelewa. Je ni vipi sisi wasichana tunaweza kuwakomesha waalimu wasitoa adhabu kali ya aina hii? |
| 62. | **CIRO** | Na pia ni vipi tunaweza kuwakomesha wazazi wasitupige? |
| 63. | **TEACHER MONA** | mmmmhhhh …sina habari kuhusu kuwepo kwa adhabu ya aina hii shuleni..? |
| 64. | **FATUMA** | Lakini waalimu wengine wanatekeleza adhabu hii.Katika shule nyingine pia waalimu wanaruhusiwa kutoa adhabu hii. |
| 65. | **CHEPTOO** | Mwalimu Mona, sasa kuna haja gani ya kujadili hoja hii katika bunge letu la wasichana?' Hakuna haja!. |
| 66. | **TEACHER MONA** | Wasichana, msife moyo. Twendeni kumuona afisa Janet. Labda atakuwa na ushauri zaidi. |

67. **NARRATOR** Na hapo Mwalimu Mona na wasichana hao wanakwenda moja kwa moja hadi ofisini kwa Afisa Janet kupata ushauri zaidi katika juhudi za kutafuta njia bora kukomesha udhalimu dhidi ya wasichana. Afisa Janet anakwenda kulijadilia suala hili na Mwalimu mkuu na hatimaye mwalimu mkuu anaitisha kikao cha dharura cha Waalimu wote.

**SCENE 5 STAFF MEETING**

**68. SFX: teachers voices in the background (studio)**

69. _**HEADMASTER** Kama mwalimu mkuu, kuna suala muhimu amablo limewasilishwa na Afisa wa masuala ya Jamii Bi Janet. Na suala hili ndio ajenda yetu kuu.Hivyo basi nachukua nafasi hii kumualika Bi Janet.

70. **JANET** Waalimu, nimefahamishwa kwamba baadhi ya wanafunzi wanapewa adhabu kali ya kutandikwa viboko shuleni. Lakini si kosa lenu kwani nyinyi pia mulipitia hayo wakati mlipokuwa shuleni.

71. **STAFF** Ni kweli ... ni kweli kabisa

| | | |
|---|---|---|
| 72. | **JANET** | Lakini sasa mambo yanaendelea kubadilika. Kulingana na shirika la Umoja wa mataifa la kupigania haki za Watoto, UNICEF,kutumia kiboko, kofi au mateke kama mbinu ya kumuadhibu mtoto ni ukiukaji wa haki zao. |
| 73. | **HEADMASTER** | Kwa hiyo unamaana kwamba Watoto wasichukuliwe hatua za kinidhamu.? |
| 74. | **JANET** | Hapana..hapana…ni lazima tudumishe nidhamu miongoni mwa watoto wetu. Lakini sikusema kwamba tutumia mbinu zinazokiuka haki za watoto hawa katika kuwaadhibu.Tunayo nafasi ya kuwauliza watoto wenye, wanavyotaka kuadhibiwa… Labda wanamaoni mazuri zaidi katika kudumisha nidhamu miongoni mwao!! |
| 75. | **NARRATOR** | Wazo zuri ! Hii ni hoja muafaka kujadiliwa katika bunge la Wasichana.Tunacho subiri ni kuona iwapo Watoto watajitokeza na mbinu mbadala ya kuadhibiwa mbali na ile ya kutandikwa. |

**SCENE 6 GIRLS PARLIAMENT**

**76. SOUNDS: MURMURINGS FROM GROUP OF CHILDREN**

| | | |
|---|---|---|
| 77. | **CHEPTOO** | Kimya!!! Kimya nyote, bunge la wasichana limemwalika hapa kwasababu hatutaki tena adhabu ya kutandikwa viboko, makofi au mateke.. |
| 78. | **CHILDREN** | Wambie ….wambie ….. |
| 79. | **CHEPTOO** | Hivi majuzi Fatuma, ailitandikwa shuleni na hata nyumbani pia. Labda tusikie maoni yake kama ungeliuzwa, ungepende kuadhibiwa vipi? |
| 80. | **FATUMA** | Kwanza ni na haki ya kupata usingizi wa kutosha kama watoto wengine. Pili mwalimu anieleze sababu za kuniadhabu kabla ya kufanya hivyo na pia kwanza anipe nafasi ya kujieleza.Na iwapo nitapatikana na hatia, basi Mzazi wangu apewa nafasi ya kwanza ya kuniadhibu kwa kuninyima huduma vitu vilivyo na umuhimu mkubwa kwangu … mfano kunificha rinda langu ninalolipenda kwa muda wa miezi michache. |
| **81.** | **SFX: CLASS** | **All CLAP** |

| | | |
|---|---|---|
| 82. | **CHEPTOO** | Na wewe Abdi? |
| 83. | **ABDI** | Mimi hupenda sana kucheza mpira na wavulana wengine kijijini. Na iwapo nitakuwa nimekosa basi wazazi wangu wanaweza kunikataza kutoka nje kuchezo mpria kwa siku chache.Kwa kufanya hivyo nitafahamu makosa yangu na kujirekebisha. |
| **84.** | **SFX: CLASS** | **CLAP** |
| 85. | **CHEPTOO** | Na wewe Ciro? |
| 86. | **CIRO** | Nikiwa darasani na nimekosa kufika kiwango cha kuadhibiwa, mimi ni mzungumzaji sana, Mwalimu anaweza kunitenga pembeni nisizungumze na Mtu yoyote kwa muda wa tusema saa moja. Hivyo nitahisi kwamba kweli nimeadhibiwa. |
| 87. | **CHEPTOO** | Inavyoonekana ni kwamba kuna maoni mengi tunayoweza kutoa kwa waalimu na wazazi. Sasa Ciro umejaribu kuyachambua? |

**88. NARRATOR** Nani aliyedhani kwamba Watoto wangeweza kutoa maoni mazuri kama haya kuhusu mapendekezo ya jinsi wangependa kuadhibiwa kwa makosa wanayotenda!! Ni matumaini yetu kwamba waalimu watayatekeleza mawazo haya badala ya kutumia kiboko.

**SCENE 7 FATUMA'S PARENTS HOMESTEAD**

**89. SFX: Outside Atmosphere, birds. People from afar**

90. **ELDER JACOB** Janet.. unaitwa Janet sivyo? Yule afisa wa masuala ya jamii? Nini kinachokuleta hapa?

91. **JANET** Mzee Jacob, nafurahi kwamba unanifahamu vyema,na mimi sikuja hapa kugombana na wewe.

92. **FATUMA** Baba, Janet amekuja hapa kushauriana nawe kuhusu mbinu bora za kuniadhubu ninapokosa.

93. **ELDER JACOB** Hilo ni rahisi.Nitakuchapa kofi ndio utashika adabu yako.Hii ndio adhabu nzuri sana na ilifaulu wakati Babangu alikuwa akinitandika makofi na kunipiga mateke kila mara ninapokosa.

| | | |
|---|---|---|
| 94. | **JANET** | Lakini sasa mambo yamebadilika mzee Jacob. Zipo njia nyingine za kutoa adhabu bila ya kumpiga Mtoto.Kwani kwa kufanya hivyo ni dhulma dhidi ya watoto. |
| 95. | **ELDER JACOB** | Sasa unanifunza jinsi ya kuwalea watoto wangu? |
| 96. | **JANET** | Hapana …Hapana..Mzee Jacob.Na si madhumuni yangu kuchukua jukumu la kuwalea watoto wako. Ninachotaka ni kukuomba tu uwape nafasi Fatuma na Mamake kushauriana nawe kuhusiana na mbinu bora za kumuadhibu Fatuma anapokukosea.Hivyo tu.. na nakuomba uwasikilize. |

**97. Theme music**

**98. OUTRO**

99. **NARRATOR**

Kumbadilisha Mtu nia huwa si kazi rahisi, na si jambo linalowezekana mara moja. Huenda itachukua muda lakini msingi ni kamba Watoto  sasa wanaufahamu kuhusiana na haki zao.Na pia wanajaribu kupaza sauti zao. Ni hayo tu kwa kipindi cha Leo cha Noa Bongo Jenga Maisha yako. Iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe  Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.